**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1500
*Mitazamo ya Ontolojia ya Waswahili katika Riwaya Teule za Muhammed Said Abdulla*

# Mitazamo ya Ontolojia ya Waswahili katika Riwaya Teule za Muhammed Said Abdulla

**Tatu Y. Khamis**
*Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-06-17
Kurekebishwa: 2025-09-20
Kukubaliwa: 2025-12-22
Kuchapishwa: 2025-12-23

**Maneno Muhimu**
Mitazamo
Ontolojia
Riwaya
Waswahili

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Khamis, T. Y. (2025). Mitazamo ya Ontolojia ya Waswahili katika Riwaya Teule za Muhammed Said Abdulla. *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 3*(2), 128-137.

Copyright © 2025
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Makala hii inafafanua namna mitazamo ya jamii ya Waswahili katika riwaya teule za Muhammed Said Abdulla (kuanzia sasa ataitwa MSA) inavyostawisha ontolojia yao. Kuwapo kwa suala la mitazamo tofauti katika jamii ya Waswahili limekuwa likishughulisha watafiti wengi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa kila jamii ina namna yake ya kuangalia mambo kulingana na vyanzo vyao vya epistemolojia ambavyo kwavyo ontolojia huzaliwa (Sanga, 2018; Khamis, 2022). Hata hivyo, suala hili limekuwa likijadiliwa katika ujumuishi wa Uafrika bila ya kuangalia jamii pwekepweke. Makala hii inabainisha namna riwaya za MSA zinavyodhirisha kuwa mitazamo ya Waswahili ndiyo inayostawisha ontolojia yao. Makala hii imetokana na usanifu wa uchunguzi kifani ambapo data zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini. Kupitia mbinu hiyo, jumla ya riwaya tatu (3) zimesomwa na kuchambuliwa. Riwaya hizo ni: *Kisima cha Giningi* (2011), *Duniani Kuna Watu* (2017) na *Kosa la Bwana Msa* (2013). Nadharia ya Ndani-Nje imetumika kwa kukamilishana na mbinu ya usimbishaji wa kimaudhui. Matokeo yanadhihirisha kwamba kuna mitazamo mitatu ya ontolojia ya Waswahili. Mitazamo hiyo ya kiontolojia ni: mtazamo wa imani za kijadi, mtazamo wa imani za kidini na mtazamo wa imani changamani.

## Utangulizi

Katika kazi za kifasihi husawiriwa mambo ya jamii ambayo kila jamii huyaagalia kwa namna yake (Sanga, 2021). Uangaliwaji huo hutokana na chukulizi za jamii husika kulingana na falsafa yao. Chukulizi hizo hutambulika kama mtazamo. Kwa mujibu wa BAKITA (2015) mtazamo ni mawazo aliyonayo mtu kuhusu suala fulani. Hapa ina maana kwamba fikra za watu kuhusu jambo la jamii husika hutofautiana kutoka jamii moja na nyingine kulingana na tajriba walizonazo. Miongoni mwa tajriba za watu ni fikra kuhusu suala la ontolojia.

Dhana ya ontolojia inarejelea kuwapo kwa mtu, jamii na ulimwengu kwa jumla, sababu na hatima yake (Temples, 1959; Mbiti, 1969; Mulokozi, 2017). Akizungumzia suala la kuwapo, Sengo (2009) anasema kuwa, kimantiki, kuna hali mbili zinazoelezea kuwapo kwake. Hali hizo ni hali ya "kuwapo kwa lazima" ambayo hutegemea chanzo asilia; na hali ya "kuwapo kusiko kwa lazima" ambayo hutegemea haja za mzunguko wa kuwapo. Kwa makala hii, dhana ya ontolojia imerejelea kuwapo kwa mtazamo na imani kuhusu jamii na mazingira yanayoizunguka. Jamii inayorejelewa hapa ni jamii ya Waswahili na mitazamo yao.

Waswahili ni watu wanaopatikana pwani ya mwambao wa Bahari ya Hindi. Hapa tunamaana kwamba ni wale wanaoanzia Kaskazini mwa pembe ya Afrika na Kusini mwa Msumbiji (Sengo, 2009; Jumanne, 2025). Jamii hizi pia hupatikana katika maeneo kama vile Kenya, Uganda na

Tanzania (Mulokozi, 2017). Waswahili wanaozungumziwa katika makala hii ni wale wamilisi wa lugha ya Kiswahili ambao wameathiriwa na mila, desturi na itikadi za jamii yao (Ponera, 2024). Watu hao wana fasihi yao ambayo hudhihirisha mitazamo yao kupitia tanzu mbalimbali ikiwamo riwaya.

Riwaya ni utanzu wa fasihi ambao unatoa nafasi pana ya kusawiri mambo ya jamii husika kwa kufafanua mitazamo ya jamii hiyo (Mlaga, 2017, Mulokozi, 2017). Kutokana na hili imeonekana kuwa ipo haja ya kuchunguzwa kwa mitazamo ya ontolojia ya Waswahili katika riwaya za MSA ili kufafanua namna mitazamo hiyo inavyosimamia ontolojia yao.

**Maelezo Mafupi kuhusu Riwaya ya *Kisima cha Giningi***

Riwaya ya *Kisima cha Giningi* imeandikwa na MSA na kuchapishwa kwa mara ya kwanza na *Evans Brothers Kenya Limited* nchini Kenya. Toleo hili lililotafitiwa, limechapishwa mwaka 2011. Riwaya hii inahusu harakati za wanakijiji wa Giningi wanazozifanya huku wakitegemea kisima cha Giningi kama chanzo chao cha maji kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao ya kila siku. Mwandishi anasawiri imani za kishirikina katika kijiji cha Giningi, ambapo wananchi wake wanaona suala hilo ni muhimu kumaliza shida zao.

**Maelezo Mafupi kuhusu Riwaya ya *Duniani Kuna Watu***

*Duniani Kuna Watu* ni riwaya iliyoandikwa na MSA na kuchapwa mara kadhaa. Toleo lililotafitiwa limechapishwa na *East African Educational Publishers Ltd* mwaka 2017. Riwaya inahusu maisha ya Bw. Hakimu Marjani na familia yake yenye watoto wawili, Kasim na Selume. Riwaya inasawiri malezi ya Bw. Hakimu kwa watoto wake kiasi ambacho anawapa kila kitu ili wasipate shida. Aidha, inaoneshwa namna watu wanavyoamini kuhusu *Kurani* kama kiongozi chao katika kutatua masuala yao yanayowasibu.

**Maelezo Mafupi kuhusu Riwaya ya *Kosa la Bwana Msa***

*Kosa la Bwana MSA* ni riwaya iliyoandikwa na MSA na kuchapishwa mwaka 2013 na *Vide~Muwa Publishers Ltd*. Riwaya hii inahusu masuala ya dini, mapenzi na ndoa, wivu na upelelezi. Masuala hayo yamejadiliwa kwa kiasi kikubwa kupitia wahusika kama vile Bwana Msa, Jamila, Bwana Ahmed Soud (Bwana Ali Soud), Tunu, Bi. Shinuna na Sheikh Judi. Kwa jumla, riwaya imeonesha namna Bwana Ahmed Soud alivyojipa majina mawili katika miji miwili tofauti ili aweze kumficha mke wake kuwa yupo peke yake katika ndoa yao.

**Nadharia Iliyotumika**

Nadharia ya Ndani-Nje ndio iliyotumika kama mwongozo katika uchanganuzi wa data za makala hii. Nadharia ya Ndani-Nje ni nadharia iliyoasisiwa na Sengo miaka 1980 (Khamis, 2022). Msingi wake mkuu ni ukweli ambao mtu akiuhitaji kuupata katika kuhakiki au kuchambua kazi za kifasihi basi lazima aisaili jamii husika ili aupate ukweli huo. Kwa mujibu wa Khamis (2022) misingi mingine ni: mosi, ili kuijua fasihi ya watu ni muhimu kwanza kuwajua watu wenyewe. Hii ina maana kwamba, ili mtu awajue watu, ni lazima aishi au kuzungumza nao. Hii ni kwa sababu mtu huyo ataweza kuelewa mambo muhimu ambayo kwayo jamii hiyo hujipambanua. Msingi wa pili ni kuwa, mambo ya jamii sharti yazingatie kweli za ndani ya jambo. Kweli hizo hujengwa na vipengele kama vile uzazi, malezi, mavazi, na imani za dini ambazo huziamini. Msingi wa tatu ni kuwa, itikadi na imani za watu zina nafasi kubwa katika kuathiri maisha na maendeleo yao. Hivyo, ni lazima zizingatiwe ili zisaidie katika kutambua mitazamo inayojenga maisha yao. Msingi wa nne unasema kuwa, mitazamo ya jamii hutokana na fani walizo nazo ambazo hutumika kuitambulisha jamii yao. Kwa makala hii, msingi wa pili na wa tatu ndio iliyotumika katika kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha matokeo ya makala hii. Nadharia hii imekamilishana vyema na usanifu, usampulishaji na mbinu ya uchanganuzi kwa sababu ukweli unaopatikana katika jamii ya

Wazanzibari kuhusu mitazamo yao iliwekwa pamoja, huku ikithibitishwa na riwaya teule za MSA kama kifani cha riwaya za Kiswahili katika jamii ya Waswahili.

**Methodolojia**

Data zilizozalisha makala hii zimepatika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini ambapo riwaya tatu za MSA zimesomwa na kuchambuliwa. Riwaya hizo ni *Kisima cha Giningi* (2011), *Duniani Kuna Watu* (2017) na *Kosa la Bwana Msa* (2013). Uchanganuzi wa kimaudhui ulitumika ambapo data zilizofanana zimewekwa pamoja ili kukidhi haja ya makala husika. Pamoja na mbinu hiyo misingi ya nadharia ya Ndani-Nje imekamilishana katika kufafanua namna riwaya za MSA zinadhihirisha mitazamo ya jamii ya Waswahili ambayo inaimarisha ontolojia yao. Data ziliwasilishwa kimaelezo kutokana na utafiti uliofanyika ulitumia mkabala ya kitaamuli.

**Matokeo ya Utafiti**

Sehemu hii inafafanua matokeo ya utafiti uliofanywa kuhusu namna riwaya teule za MSA zinavyodhihirisha mitazamo ya ontolojia ya Waswahili. Data zimeonesha kuwa kuna mitazamo mitatu katika jamii ya Waswahili inayoongozwa ontolojia yao. Mitazamo hiyo ni: mosi, mtazamo wa imani za kijadi. Pili, ni mtazamo wa imani za kidini na tatu, ni mtazamo wa imani changamani.

**Mtazamo wa Imani za Kijadi**

Dhana ya ujadi inarejelea utumiaji wa vionjo vya asili ambavyo hufungamana na jamii husika (Ponera, 2014). Imani za kijadi ni mtazamo wa imani za asili ambao ulikuwapo katika jamii za Waafrika kabla ya kuingia kwa wageni (Mulokozi, 2017; Hassan, 2018). Kwa mujibu wa Mulokozi (2017), mtazamo huu hufungamanishwa na mazingira ya jamii husika, ndio maana masuala kama mizimu, miti na majabali hujumuishwa katika ibada za watu. Waswahili wanaamini kuwa, mtazamo wa imani ya kijadi ni mtazamo ambao watu huamini na kufuata imani za kiasili. Imani hizi hujumuisha utambikaji, kuamini mizimu, mashetani na majini. Kwa makala hii tutazungumzia itikadi, mizimu na majina ya mitaa.

MSA ameyasawiri masuala ya kiitikadi katika riwaya zake kwa kudhihirisha mtazamo wa kijadi katika ontolojia ya Waswahili. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, ameonesha jinsi watu wanavyochukua nguo za wenzao na kuzikata vipande ili wakawaroge (uk. 13). Pia, mwandishi amemsawiri Bwana Ali Makame kuwasilisha watu waliopo katika jamii ya Waswahili wanaofanya ubaya kwa wenzao. Hii ni kwa sababu Bwana Ali Makame alienda kwa mganga kwa ajili ya kumroga mwanawe kwa lengo la kupata urithi. Haya yanabainika pale fundi Mangungu anapozungumza na Bwana Msa na kusema, "Juzi hapa kaja yeye Ali Makame kumloga mwanawe, mwana wa nduguye, atokane na mumewe na yamfike ya kumfika ili yeye arithi… (uk. 46). Dondoo hili linafafanua namna mtazamo wa kijadi unavyoimarisha ontolojia ya Waswahili katika fikra walizo nao kuhusu masuala ya urogaji. Kitendo cha Ali Makame kumroga mwanawe kinadhihirisha ukweli wa jamii hiyo kama inavyoaridhiwa na msingi wa pili wa nadharia ya Ndani-Nje unaosema kuwa mambo ya jamii sharti yazingatie kweli za ndani ya jambo. Akizungumzia suala la mtazamo wa kijadi, Kamage (2023) analihusisha sula la kurogana na nguvu-uhai za Kiafrika ambazo huwa zinahusisha uchawi na ushirikina katika jamii husika. Akitoa mfano wa jamii ya wilaya ya kati ya Unguja, Khamis (2008) anasema watu wa eneo hilo hutumia wachawi au waganga ili kurogana. Kwa mantiki hii, itikadi ya kulogana kichawi kwa kutumia waganga katika jamii ya Waswahili, inadhirisha kuwapo kwa mtazamo wa imani za kijadi katika jamii hiyo.

Aidha, kipengele kingine kinachohusiana na mtazamo wa imani za kijadi ni mizimu. Mizimu hujumuisha wahenga na mashetani ambao hawawezi kudhihirika kupitia milango mitano ya fahamu lakini wana uhusinao wa moja kwa moja na wanadamu wa jamii husika (Mnenuka, 2020). Likifafanua zaidi BAKITA (2015) linasema kuwa mizimu ni kivuli cha mtu ambaye amekwisha

fariki dunia. Hujumuisha mahali panapofanyiwa matambiko ambapo aghalabu huwa chini ya miti mikubwa kama vile mbuyu, mkuyu au pangoni kwenye mawe makubwa na marefu au mahali panapotuama maji. Katika riwaya za MSA, kuna mzimu Habusa ambao watu wanautumia katika kuomba mambo yao. Miongoni mwa mambo hayo ni kutafuta kazi, kizazi, mume au mke, kutuliza nyumba na kutoa mihanga kwa ajili ya kushukuru kutokana na yale waliyoyaomba wakayapata. Hili linadhihirika pale mwandishi anaposema:

> Watu wanaokuja kutembelea Giningi humchukulia zawadi Habusa, kama vile mayai au halua, na wakimwona, humwita, Habusa! Habusa! Zawadi yako hiyo! – na Habusa hunyanyua kichwa chake kabla zawadi hizo hazijagusa maji. Watu wengi huja kuweka nadhiri, wakaomba maombi yao wayatakayo kwa jina la Habusa, na inasemekana kuwa kila liombwalo kwa jina lake hupatikana (uk. 68).

Dondoo hili linaonesha nguvu ya mzimu unaoitwa Habusa. Mzimu unaotumiwa na watu kuomba mambo yao na kufanikiwa kwa yale wanayoyaomba. Aidha, linaonesha namna watu wanavyopeleka vishuo katika mzimu huo. Mwandishi kuonesha watu hupeleka zawadi mbali mbali inadhihirisha vishuo vinavyopelekwa kama sehemu ya shukurani kwa mzimu kufanya kazi iliyotegemewa. Kwa mantiki hiyo, mwandishi wa riwaya hii amebainisha kuwapo kwa matumizi ya mizimu katika jamii ya Waswahili. Mzimu Habusa unawakilisha mizimu mingi iliyopo katika maeneo mbalimbali katika jamii hiyo. Mizimu hiyo huombwa kwa shida mbalimbali na watu hutoa mihanga kwa ajili ya maombi au shukurani kwa kufanikiwa maombi yao. Miongoni mwa mihanga inayotolewa ni wanyama na hata mwanadamu kwa ajili ya damu yao.

Mwandishi ameonesha suala la mhanga kwa kubainisha kuwa Mwana wa Gigingi aliuliwa katika pango lililopo huko katika kisima cha Giningi. Mauaji haya yanawakilisha mihanga inayotolewa katika mizimu ambayo inahusisha umwagaji wa damu. Mwandishi anasema:

> Inasemekana kuwa tangu Habusa kuvifungua vyumba vile sita, vyumba vyote hivyo vilipotea, kikabaki chumba kile kile kimoja tu kilichomtia msichana yule hatarini. Na chumba hicho, asili yake, kilikuwa ndiko msalani, na kwa hivi sasa ndiko kunakotumika kwa kutekea maji watu wa Giningi… Na huko ndiko ilikotokea habari ya kusikitisha kuwa yule bibi mzuri aitwae Mwana wa Giningi kaonekana kafa (uk. 68).

Dondoo hili linaonesha jinsi Waswahili wanavyoamini masuala ya kijadi. Wanaamini kuwapo kwa mizimu na wanaitumia katika kufanikisha shughuli zao mbali mbali. Aidha, wanaamini katika utoaji wa mihanga kuwa ni sehemu ya kuipa nguvu mizimu yao. Akishadidia kuhusu suala hili, Khamis (2008) anatoa mfano wa namna suala la mizimu linavyojitokeza katka jamii ya Wazanzibari ambao ni sehemu ya Waswahili. Anasema kuwa uzoefu unaonesha kuwa baadhi ya maeneo ya Kusini Unguja yana tabia ya kutumia mizimu kwa kufanyiana ubaya wa kutumia punju na chui. Eneo la Kaskazini Unguja hadi Pemba wanatumia mashetani na vizuu. Hii ina maana kwamba kila eneo lina aina yake ya kufanya masuala hayo ingawa wote wanaamini katika mizimu. Kuna maeneo yanayotumia mizimu kiuchawi kwa kulogana na wengine kupeana majini na mashetani.

Kwa upande mwingine, kuwapo kwa majina ya mitaa yenye majina ya mizimu, mashetani, masharifu, mashehe, pamoja na kudhuriwa kwa manuizo (katika makaburi) kunadhihirisha kuwa katika jamii ya Waswahili kuna watu wenye mtazamo wa imani za kijadi. Kulingana na msingi wa nne wa nadharia ya Ndani-Nje, itikadi na imani za watu katika jamii zina nafasi katika kuathiri maisha yao. Ndio maana riwaya teule za MSA zimesawiri mtazamo wa imani za kijadi katika jamii ya Waswahili kwa kuwa, kulingana na mitazamo yao, huo ndio ukweli kuhusu wao. Mwandishi anasema katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*:

> Shauku ya kuzaa ilipaa ikapindukia, asisikie kwamba kuna kaburi la shehe au sharifu ila yeye atakwenda akaweke nadhiri pindi akichukua mimba atafanya jambo fulani kuhusu makaburi wa watu wale. Aliweka nadhiri kaburini kwa Mwinyi Kiemba; aliweka nadhiri kwa Sharifu Musa. Mizimu iliyoambiwa kwamba ina kabuli, yote aliifikia akaweka makafara na madhabehi (uk. 110).

Dondoo hili linathibitisha kuwa kuna majina ya maeneo ya Waswahili (Wazanzibari) yanayowakilisha majina ya mizimu. Hii ni kwa sababu, katika dondoo hilo kuna majina kama Mwinyi Kiembe na Sharifu Musa ambayo ni maeneo halisi yaliyopo Zanzibari. Mwandishi kayatumia haya kuwakilisha mengine ambayo yanapatika katika jamii husika. Kwa mujibu wa data zilizozalisha makala hii, masuala haya ndio uhalisi unaodhihirisha mitazamo ya kiontolojia katika jamii ya Waswahili. Hii ni kwa sababu nadharia ya Ndani-Nje inasisitiza kuwa, mitazamo ya jamii husika ni lazima izingatiwe ili isaidie kubaini fikra zinazojenga ontolojia yao.

**Mtazamo wa Imani za Kidini**

Mtazamo wa imani za kidini unaonekana kuwa wa kisasa ukilinganishwa na mtazamo wa imani za kijadi (Hassan, 2018). Hii ni kutokana na ukweli kwamba, imani hizi zililetwa na ustaarabu wa Kiarabu. Kwa maneno mengine, imani za mtazamo wa dini ya Uislamu imekitwa katika mafunzo ya Mtume Muhammad (S.A.W) aliyofundishwa kupitia malaika Jibril (A.S.). Hivyo, waumini wa mtazamo huu hutumia *Kurani Takatifu* kuwa ndiyo mwongozo wao (Al-Faruqi, 1992).

Data zilizozalisha makala hii zimebaini kuwa, pamoja na kuwapo kwa mtazamo wa imani za kijadi katika jamii ya Waswahili, mtazamo wa imani za kidini pia unapatikana. Hivyo, kulingana na fikra za Waswahili, ontolojia yao kwa kiasi kikubwa, imeathiriwa na kaida za dini ya Kiislamu ambapo chanzo chao kikuu cha maarifa yao ni *Kurani Tukufu*. Wanaoamini katika mtazamo huu huwa hawajishughulishi na masuala ya mashetani, vizuu wala mizimu. Wao huamini katika ibada na dua ambazo huwaongoa katika njia sahihi na dua ndizo zinazowakinga kutokana na masaibu ya dunia. Hivyo, mtu akiumwa, pamoja na kumpeleka hospitali, ni lazima wamfanyie dua. Dua zao huambatana na uaguzi wa matatizo yao lakini kwa kutumia *Kurani Tukufu*. Suala hili la kutumia *Kurani Tukufu* katika kutatua matatizo yao, limedhihirishwa na mwandishi mteule katika riwaya zake. Kwa mfano, katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, mwandishi amemsawiri Bwana Msa kutumia *Msahafu* katika kubaini mali za Bwana Hakimu Marjani zilipopotea. Anasema:

> "Alikuwa na imani kuwa Kurani takatifu itaongoza tu, haitapoteza," alijibu Bwana Msa huku akitupa mafunda ya moshi hewani. "Tukirejea katika maelezo yetu," alianza tena Bwana Msa, "niliendelea kupekua, nikakuta aya hii: *Mwenyezi Mungu anakuleteeni baa la mto wa maji*. Aya hii haina mstari chini yake ila kwenye 'mto wa maji'; kwa hivyo, mushkeli sana, haja yake ndani yake ni huo mto wa maji tu. Mahala pengine nikaona aya hii: *Kutoka mti wenye baraka, mzeituni*; na katika aya hii, 'mzeituni' tu ndio uliopigiwa mstari chini yake. Hapa akili yangu ilizua kidogo: Vipi 'mto wa maji' na 'mzeituni'? Vitu vyote viwili vinapatikana shamba. Twende. Kuendelea zaidi nikafika kwenye aya hii: *Hakika idadi ya miezi kwa Mwenyezi Mungu ni kumi na mbili*. Hapa sikuwaza sikusita sana; juu n'nayo 'shamba', hapa nimepata 'kumi na mbili', kuchanganya, akili yangu ilin'ambia; 'shamba maili kumi na mbili'; nikasema rohoni mwangu: huyu mtu alikuwa na shamba Kazole; huyu mtu aliwahi kuwa Kazole, anataka wakaulizwe wajuao, huko Kazole? Lakini Kazole nako ni maili kumi na mbili? Sijui. Lakini twende na kazi yetu ya kupekua Msahafu. Kikirikikiri, nikaipata aya hii: *Wawili (au viwili) wamo (au vimo) katika pango*. Na aya hiyo yote imepigwa mstari chini yake. Baada ya hapo nilikwisha kutafuta na kupekua zaidi

> karatasi mojamoja nisikute aya nyingine tena iliyopigiwa mstari chini yake ila hii: *Na kawaulizeni watu wa kijiji tulichokuwapo*. Mambo yamekwisha; hapana ila Kazole ni maili kumi na mbili. Niliona hivi: ikiwa Kazole nimepata haja yangu, na ikiwa si hivyo basi kazi yangu ni bure na pengine nimepoteza wakati wangu bilashi… (uk. 102).

Dondoo hili linaonesha namna Bwana Msa alivyoitumia aya za *Kurani* katika kufanikiwa kupata mali za Bw. Hakimu ambazo zilikuwa hazijulikani zilipo. Hii ni kusema kuwa dondoo linadhihirisha katika jamii ya Waswahili wapo watu wanaotumia *Kurani Tukufu* katika kutafuta au kuagua matatizo yanayowakabili, na hupata na suluhu au dawa ya tatizo hilo. Hivyo, hakuna haja ya kwenda kwa mganga wala mchawi kutafuta uaguzi kwa mashetani na mizimu.

Aidha, Waswahili wanaamini katika imani za dini kwa kutumia *Kurani Tukufu* kama chanzo chao kikuu cha maarifa yao. Hii ni kusema kuwa ndimo munamopatika miongozo yao ya ibada na dua. Kwa upande wa dua, wenye mtazamo huu wanaamini kuwa ndiyo inayomkinga mtu katika kila jambo. Dua humvua mtu katika mabalaa, maradhi na majanga. Pia, humsaidia mtu katika kutafuta riziki, kizazi, makaazi na malezi. Hivyo, wanaoamini mtazamo huu, huomba dua kila wakati kwa kuamini kuwa ndizo zitakazosaidia. Mwandishi mteule amelidhihirisha hili katika riwaya zake zilizotafitiwa. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*, mwandishi amemchora mhusika Mwanatenga akimuombea Jamila dua ya safari ili Mwenyezi Mungu ajaalie aende salama na arudi salama. Anasema, "Mungu ajaalie safari ya heri na salama; wameondoka salama, wafike salama, na waishi kwa raha" (uk. 103). Kwa uwezo wa Mungu, kweli Jamila alienda Dubai salama na kurudi salama. Hili limedhihirikia pale mwandishi anapomsawiri Jamila kumuandikia ujumbe Mwanatenga unaosema, "*Nipo dar. Kesho nakuja ndege ya saa nne*. "*Jamila*" (uk. 120). Pia, sheha wa Chwaka alimuombea dua Jamila ili aishi na mumewe vizuri. Anasema, "... Jamila ni mtoto ... kazoea sasa hapa kwangu-Mungu amweke, ampe masikilizano mema na mumewe... (uk. 14). Aidha, katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, Bwana Msa anamuombea dua Bi. Mariamu Mkembe ili Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu. Ansema, "Mungu akutawilishe umri, Bi Maryam" (uk. 102). Vilevile, Bwana Hakimu Marjani anaonekana kumuombea dua mwanawe, Selume, ili aishi vizuri na katika njia ya haki. Anasema, "... Mungu akubarikini nyote wawili, muishi kwa masikilizamo mema, mzae ndume na nke, Amin" (uk. 29).

Hali kadhalika, wenye mtazamo huu wanaamini kuwa mtu akimuombea mwenziwe dua mbaya au nzuri, Mwenyezi Mungu humjaalia kupata yeye lile aliloliomba. Hivyo, si vizuri mtu kumuombea mwenziwe dua ambayo si nzuri, dua ya kumuangamiza au ya kumuapiza. Mwandishi anathibisha hili pale Bi. Shinuna wa riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* alipomuombea mumewe Seyyid Ahmed Soud kuwa akienda Chwaka kwa mkewe mdogo basi asifike salama, apate ajali. Anasema,

> "...kama atajidai kujaribu kuja hapa, basi nakuapia Mungu, hafiki salama atakufa tu, kabla ya kufika. Na akifa yeye, bimzuri weye utakufa! Nenda wapi na wapi, lakini lazima na weye ufe. Omba salama yako wewe-mume wangu anisikilize aache kuja huku. Lakini akija, atakufa; na halafu na wewe utakufa. Kwa hali zote mbili, mimi nakutakia kuwa mume wangu humwoni tena-akisikiliza haji; akitaka kuja atakufa njiani (uk. 9)"

Dondoo hili linaonesha namna Bi. Shinuna alivyokuwa akimsimanga mke mweziwe kwa kumuombea dua mumewe kuwa akienda kwa mke huyo basi hatafika salama, lazima afe njiani. Aliyasema haya kwa kujua kuwa mpango wake utatimia wa kumuwekea majambazi mumewe ili akipita njia ya Chwaka apate ajali. Mpango huo unadhihirika katika ukurasa wa 35 pale amaposema,

> "Ndio mmefika? Aliuliza Bi. Shinuna, bibi wa nyumba ile. Sasa sikilizeni vizuri. Kesho nataka muwe makini kwa kazi yangu, mkae mahali njia kuu popote pale katika njia ya Chwaka...maana kazi yenyewe itakuwa alfajiri. Hapo mtakaa kungoja ulinzi wa gari ya maziwa-mimi sina hakika kama litapita au halipiti...Mkiliona linakuja, mtalizuia...likisimama, nyinyi msisite tena mkatia kisirani. Gari hilo likisimama tu, hapo hapo mwueni dereva wake kabla hajajua kuwa atafikwa na hatari hiyo-kisha mtoke mwende zenu" (uk 35-36).

Dondoo hili linaonesha mpango wa Bi. Shinuna wa kutaka wenziwe wafe ili yeyeabaki na mumewe peke yake. Mpango huo anauweka baada ya kumuombea dua mumewe kuwa akienda kwa mke mdogo hatafika salama. Kwa mtazamo wa imani ya dini ya Kiislamu, unalompangia mwenzio lazima likufike wewe kwanza. Ndio mana mwandishi anaonesha namna Mwenyezi Mungu anajaalia yeye (Bi. Shinuna) kupata ajali hiyo iliyosababisha kifo chake. Mwandishi anasema,

> Magharibi ilikuwa ikiingia kwa nguvu sana. Sasa, dereva wa Bi. Shinuna alikuwa akipishana na lori moja likitokea mjini, na huku hawezi kumtazama bibi yake kila anaposema. Mara alitokea ng'ombe kakata huko anafukuzwa na wenyewe Ng'ombe yule alimsanifu kuikata njia katikati. Aliweza kulipenya na kulipiga chenga lori lakini hakuweza kulipita gari la Bi. Shinuna. Katika jitihada yake ya kulipisha lori, na kutokewa na ng'ombe kwa ghafla, dereva wa Bi. Shinuna alibabaika, ukamtoka utawala wa uzuifu wa gari. Shuwari ...Alimteka Ng'ombe mzimamzima akamweka juu ya funiko la mbele linalofunika mashine, akachupa naye pamoja, ng'ombe na gari, kuangukia gengeni, genge ambalo lilikuwa kubwa wala halikuwa na kizuwizi chochote. Pale pale walipotega Joka na Shoka mtego wa kumwua Seyyid Ahmed bin Soud (mume wa Bi. Shinuna) kwa kumtupa gengeni yeye na gari lake! Tofauti yao ni wakati tu. Wale ilikuwa alfajiri, mwangaza haujazagaa; na hawa ilikuwa magharibi giza linakomaa (uk. 85).

Dondoo hili linaonesha mazingira ya ajali aliyoipata Bi Shinuna mahala palepale alipompangia mumewe afe na kumuombea dua kuwa asifike salama aendako. Hatimae yeye mwenyewe anapata ajali hiyo na kufa kama anavyosema mwandishi, "*PALEPALE ...AKIENDA CHWAKA AFAJIRI, akakutana na hatari ya kutaka kuuliwa. Bibi alikuwa AKIRUDI KUTOKA CHWAKA MAGHARIBI akakutana na ajali yake ya kufa* (uk. 86-87)". Dondoo hili linadhihirisha mtazamo wa imani ya dini ya Kiislamu iiliyopo katika jamii ya Waswahili kuwa unalomuombea mwenzio liwe zuri au baya basi MwenyeziMungu hukupa wewe kwanza. Kwa fikra za msingi wa tatu wa nadharia ya Ndani-Nje imani za watu ndizo zinazoimarisha mitazamo yao. Hivyo, mtazamo wa dini ya Kiislamu unasisitiza watu kuombeana yaliyo mema, kheri na yale mazuri ambayo hata yeyote anayapenda ayapate katika nafsi yake.

Nyongeza ya hayo, mtazamo huu unaamini kuwa nadhiri, viapo na kila jambo analofanya mwanadamu anatakiwa amshirikishe Muumba wake kwa maana ndiye anayeiendesha dunia. Hivyo, mtu akitaka kuanza jambo, huanza na jina la Muumba wake kwa kusema '*Bismillah*'. Wanaamini kuwa neno hili humfanya Muumba kuwa pamoja na mtu huyo mpaka amalize jambo lake. Mwandishi anasema, katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*: "Nadhani hata hawakujali kupiga bismillah (uk. 34)". Hapa anaonesha kuwa kuna umuhimu wa kila unalolianza utaje jina la Muumba wako kwani yeye ndiye awezaye kukuongoza katika jambo hilo. Hii ni kwa sababu Mungu ndiye atoaye riziki; hivyo, kila ukimuomba, hukuongezea.

Kwa jumla, mtazamo wa imani ya kidini humfanya mwanadamu awe karibu sana na Muumba wake. Hivyo, Mwenyezi Mungu humpa kila anachohitaji, kwa sababu anawapenda sana wanaomuomba. Kwa mtazamo huu, matumizi ya mashetani, vizuu na mizimu ni imani za kishirikina. Hivyo basi, ni makosa kumshirikisha Muumba na vitu vingine alivyoviumba. Hii ni kwa sababu kuwapo kwake ni kwa lazima, hakumaliziki wala hakutabiriki, tofauti na alivyoviumba (Sengo, 2009). Ndiyo maana wenye mtazamo huu wanasisitiza ibada na dua. Hata kama mtu ana nadhiri, basi ataweka kwa ajili ya Muumba wake, kama alivyofanya sheha wa Chwaka katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* kwa kusema, "Na mimi naweka nadhiri, Bwana Msa," alisema sheha kwa sauti iliyonyesha matumaini mema, "nitasoma Maulidi ya Mtume – pindi Mungu akinifariji akanivua salama katika baa na balaa hili" (uk. 47). Hapa sheha anaweka nadhiri ya maulidi ya Mtume kwa sababu Mtume ndiye mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Hivyo, anaweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu, si kwa shetani wala mzimu. Hivi ndivyo wafanyavyo wanaoongozwa na mtazamo wa kidini kwa kuwapo kwao. Kwa msingi wa nadhari ya Ndani-Nje, ibada na dua ndizo zinazojenga imani za Waswahili ambazo zinadhihirisha mtazamo wa ontolojia yao. Hii ina maana kwamba ulimwengu wao unabainishwa na imani zao zinazodhihirisha mitazamo ya kuwapo kwao.

**Mtazamo wa Imani Changamani**

Miongoni mwa mitazamo ya ontolojia ya Waswahili ni mtazamo changamani ambao hujumuisha vipengele vya mtazamo wa imani za kijadi na mtazamo wa kidini. Mtazamo huu, kulingana na data, ndio unaotumiwa na watu wengi zaidi kuliko mitazamo mingine (Khamis, 2022). Hii ni kwa sababu watu wengi katika jamii ya Waswahili wanaamini kuwapo kwa Muumba wao lakini wanapopatwa na matatizo, huenda kwa waganga, wachawi na mizimuni kutafuta utatuzi wa matatizo yao (Hassan, 2018; Khamis, 2022). Waganga wanaotumika hapa, kwa kiasi kikubwa, ni wale wa kijadi. Waganga hawa hutumia taaluma za kijadi katika kutibu watu kwa kutumia dawa za miti shamba, majini, mashetani, wanyama, ndege, na baadhi ya vitu vilivyomo katika mazingira yao ili kutatua matatizo yanayowakabili watu (Khamis, 2008; Mohammed, 2014; Hassan, 2018; Migodela, 2020) Wakati mwingine, waganga wa kijadi huopoa watu waliochukuliwa kimazingara, hufunga nyumba, shamba, biashara, miili na wake zao (Khamis, 2022).

Kwa kulitambua hili, MSA amesawiri matumizi ya mizimu, mashetani na majini katika riwaya zake kama tulivyowisha jadili hapo juu. Pia, ameonesha imani ya kuwapo kwa Mwenyezi Mungu, kufanya ibada na dua katika jamii hiyohiyo. Hii ni kudhihirisha kuwa, katika jamii ya Waswahili, kuna mtazamo changamani kuhusu kuwapo na mazingira yao yanayowazunguka. Kwa mfano, Mwanatenga wa riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*, pamoja na kuwa ni Muislamu, tena amesoma elimu ya dini na dunia, bado amesawiriwa kuamini itikadi za kijadi za kuamini mitego na nuhusi zinazoweza kuwapata watu wa ukoo mmoja walionuiziwa ubaya sehemu fulani. Anasema, "… pengine pahala hapo pamenuiziwa nyinyi msipite kwa salama kwa wakati huo…" (uk. 98). Maneno haya yanadhihirisha kuwa Mwanatenga ana fikra za kishirikina kwa sababu anaamini itikadi na mila za kijadi. Aidha, katika riwaya ya *Kisima cha Giningi* kumesawiriwa waganga, wachawi, mizimu, mashehe, kulogana na maombi ya dua. Haya yote yanadhihirisha uchangamani mkubwa ulipo katika jamii ya Waswahili katika kuamini kuwapo kwao na vyanzo vyao vya maarifa. Ndiyo maana wengine huitumia Kurani na wengine mizimu.

Mbiti (1969) anaona kuwa waganga wa kijadi ni watu waliopewa nguvu za kufahamu matatizo yanayowakabili watu wengine na kuweza kuyatatua. Waswahili wengi wanaamini Mwenyezi Mungu na wakati huo huo wanaamini imani zao za kijadi (Hassan, 2018). Hii ni kusema kuwa Waswahili wanasali, wanafunga na kufanya dua kama matakwa ya imani yao ya Uislamu lakini pia wanaenda kwa waganga, mizimuni na kufanya matambiko mbali mbali kama sehemu ya ujadi wao (Khamis, 2022).

**Hitimisho**

Katika makala hii imebainika mitazamo mitatu ya ontolojia ya jamii ya Waswahili kama ilivyosawiriwa katika riwaya za MSA. Pamoja na kuwa mitazamo hiyo ipo mitatu, lakini kwa kiasi kikubwa mtazamo changamani ndio unaoongoza ontolojia ya jamii husika. Hii ni kwa sababu watu wengi wanaamini katika ibada, dua, mizimu, mashetani, uganga na uchawi. Hivyo, wanamuabudu Muumba wao pamoja na mizimu yao. Makala hii sio mwisho wa utafiti kuhusu mitazamo ya jamii ya Waswahili. Hii ni kwa sababu jamii ya Waswahili ni pana. Hapa tumetumia kifani cha jamii ya Wazanzibari. Makala nyingine zinaweza kuzungumzia jamii nyingine, zinaweza zikawa na fikra tofauti kulingana na epistemolojia zao. Inapendekezwa kuwa ni vyema kuangaliwa jamii pwekepweke kwa sababu kila jamii ina chukulizi zake kuhusu mitazamo husika ya kiontolojia. Hii ni kusema kuwa inawezekana mitazamo hii ikapatikana katika jamii nyingi za Kiafrika, lakini fikra za watu kuhusu mitazamo hiyo ikatafautiana kutoka jamii moja na nyingine ndani ya Afrika kulingana na epistemolojia zao.

**Marejeleo**

Abdulla, M. (2011). *Kisima cha Giningi*. Evans.

Abdulla, M. (2013). *Kosa la Bwana Msa*. Masomo Bookshop.

Abdulla, M. (2017). *Duniani Kuna Watu*. East African Publishing House.

Al-Faruqi, I. (1992). *Al Tawhid: Its Implications for Thought and Life*.Virginia International Institute of Islamic Thought Publication.

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Longhorn Publishers Limited.

Haji, G. (2015). Mbinu za Utunzi wa Nyimbo za Uganga wa Pepo Zanzibar: Mifano kutoka Jamii ya Watumbatu. *Kioo cha Lugha*, 13 (1), 7-27. https://journals.udsm.ac.tz.

Hassan, R. (2018). Ujaala katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka *Tungizi za Mnyagatwa* na *Diwani ya Midulu* (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.) https://repository.udom.ac.tz.

Jumanne, A. (2025). Usawiri wa Ukizinda kwa Mawanda ya Mtu katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutokaa *Rosa Mistika* na *Harusi*. *Nuru ya Kiswahili*, 4(1), 58-85. https://DOI.org/10.58548/2024nuru41.5885.

Kamage, A. (2023). Usawiri wa Nguvu-uhai katika Jamii za Kiafrika: Mifano kutoka Riwaya ya *Mzishi wa Baba Ana Radhi*. *Mwanga wa Lugha*, 8(1), 37-48. Kaponda, G. (2018). *Ontolojia ya Kiafrika katika Mbolezi za Wanyasa* (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma). https://repository.udom.ac.tz.

Khamis, A. (2008). Jadi na Utamaduni wa Mswahili wa Zanzibar katika *Utamaduni wa Mzanzibari* (1-22). BAKIZA.

Khamis, T. (2022). *Mdhihiriko wa Ontolojia ya Wazanzibari katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano Kutoka Riwaya Teule za Muhammed Said Abdulla* (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma). https://repository.udom.ac.tz.

Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Mture Education Publishing Limited.

Makame, S. (2016). *Matumizi ya Falsafa ya Usihiri katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi*. (Tasinifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma). https://repository.udom.ac.tz.

Mbiti, J. (1969). *African Religion and Philosophy*. Heineman.

Migodela, W. (2020) *Kuchunguza Mtindo katika Nyimbo za Tiba Asilia: Mifano Kutoka Nyimbo za Waganga wa Mkoa wa Ruvuma* (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). https://repository.out.ac.tz.

Mlaga, W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Heko Publisher Limited.

Mnenuka, A. (2020). Mizimu katika Ngano za Kiafrika: Uchambuzi wa Ngano teule. *Mulika* 39, 1-19.

Mohamed, I. (2014). *Mchango wa Nyimbo za Ngoma ya Mdatu katika Kudumisha Maadili ya Watu wa Mafia* (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma). https://repository.udom.ac.tz.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu.* Moccony Printing Press.

Ponera, A. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Karljamer Printing Technology.

Ponera, A. (2024). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Shareef Printers.

Sanga, A. (2018). *Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Andishi za Kiswahili Kipindi cha Utandawazi: Mifano ya Hadithi Fupi kutoka Magazeti ya Habari leo, Nipashe na Mwananchi ya Mwaka 2008 Hadi 2014* (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma). https://repository.udom.ac.tz.

Sanga, A. (2021). Thamani ya Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Simulizi za Kiswahili. *Mulika*, 40(1), 108-125. https://journals.udsm.ac.tz.

Sengo, T. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. AERA Kiswahili Research Product.

Temples, P. (1959). *Bantu Philosophy* (C. King, Trans.). Présence Africaine.